**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA UTALII NA MAMBO YA KALE

## MHESHIMIWA LELA MUHAMED MUSSA (MBM)

## KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA, AKIWASILISHA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**MEI, 2021**

**YALIYOMO**


YALIYOMO……………………………………………………………………...i

VIFUPISHO VYA MANENO……………………………………………………….iv

A. UTANGULIZI……………………………………………………………....1

B. MUUNDO WA WIZARA..........................................................................3

C. MAJUKUMU YA WIZARA.......................................................................4

D. PROGRAMU KUU ZA WIZARA..............................................................4

E. UTALII NA UCHUMI WA BULUU.............................................................5

F. MCHANGO WA SEKTA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KATIKA MAENDELEO YA NCHI.............................................................................6

G. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.................................................................................................7

H. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021......................................................................................8

I. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021......................................................................12

PROGRAMU KUU – KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII………....12

PROGRAMU KUU – MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE.............................................14

PROGRAMU NGODO – UENDELEZAJI WA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE.........................................15

PROGRAMU NDOGO – UHIFADHI WA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA..........................................................................................19

PROGRAMU KUU – UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI WA UTALII..21

PROGRAMU KUU – KURATIBU NA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII.......................................................................................................23

PROGRAMU KUU – UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA UTALII NA MAMBO YA KALE..................................................................26

PROGRAMU NDOGO – UTAWALA NA UENDESHAJI KATIKA SEKTA YA UTALII NA MAMBO YA KALE..........................................................27

PROGRAMU NDOGO – KURATIBU NA KUSIMAMIA MIPANGO MIKUU YA WIZARA...................................................................................28

PROGRAMU NDOGO - KURATIBU NA KUSIMAMIA UTAWALA, UENDESHAJI NA MIPANGO YA OFISI KUU – PEMBA..........................30

J. MIRADI YA MAENDELEO ITAKAYOTEKELEZWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022...................................................................32

K. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022...........33

L. KUWASILISHA BAJETI YA MFUMO WA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA2021/2022........................................................................34

PROGRAMU KUU – KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII................35
PROGRAMU KUU – MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE................................................36
PROGRAMU NGODO – UENDELEZAJI WA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE.........................................36
PROGRAMU NDOGO – UHIFADHI WA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA........................................................................................37
PROGRAMU KUU – UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI WA UTALII..38
PROGRAMU KUU – KURATIBU NA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII..........................................................................................39
PROGRAMU KUU – UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA UTALII NA MAMBO YA KALE...................................................40
PROGRAMU NDOGO – UTAWALA NA UENDESHAJI KATIKA SEKTA YA UTALII NA MAMBO YA KALE.............................................41
PROGRAMU NDOGO – KURATIBU NA KUSIMAMIA MIPANGO MIKUU YA WIZARA.........................................................................42
PROGRAMU NDOGO - KURATIBU NA KUSIMAMIA UTAWALA, UENDESHAJI NA MIPANGO YA OFISI KUU – PEMBA...........................43
M. SHUKURANI...........................................................................................44
N. MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022........................................45
O. HITIMISHO.............................................................................................46
VIAMBATISHO.........................................................................................47
1A. MCHANGANUO WA FEDHA KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU..........................................................................................48
1B. MCHANGANUO WA FEDHA KWA TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU..........................................................................................49
1C. MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI HADI MACHI 2021.....................50
1D. FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 KWA KILA PROGRAMU NDOGO.........................................................................51
1E. FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 KWA KILA PROGRAMU NDOGO.........................................................................54
1F. BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWA TAASISI ZISIZO ZA RUZUKU........................................56
1G. BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWA TAASISI YA RUZUKU.........................................................58
1H. BAJETI INAYOOMBWA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWA KILA PROGRAMU NDOGO.....................................................................59
1I. MAKADIRIO YA MAPATO YANAYOINGIA HAZINA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022...................................................................................62

2. WAFANYAKAZI WA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE WALIOKWENDA MASOMONI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021……...................................................................................63
3. ORODHA YA NYUMBA NA WAMILIKI ZILIZOPO MJI MKONGWE.....65

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| **ASP** | Afro Shirazi Party |
| **CCM** | Chama cha Mapinduzi |
| **CFR** | Centre for Foreign Relation |
| **DKT** | Daktari |
| **FM** | Frequency Modulation |
| **GDP** | Gross Domestic Product |
| **IAA** | Institute of Accountancy Arusha |
| **ICPS** | Institute of Continuing and Professional Studies |
| **IPA** | Institute of Public Administration |
| **KTN** | Kenya Television Network |
| **KLM** | Koninklijke Luchtvaart Maatschappij |
| **KIST** | Karume Institute of Science and Technology |
| **LEO** | Labour Empowerment Organization |
| **MBM** | Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi |
| **MNMA** | Mwalimu Nyerere Memorial Academy |
| **NTV** | Nation TV |
| **OUT** | Open University of Tanzania |
| **PBB** | Program Based Budget |
| **PBZ** | People Bank of Zanzibar |
| **SMT** | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| **SMZ** | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| **SUZA** | State University of Zanzibar |
| **TBC** | Tanzania Broadcasting Cooperation |
| **TSH** | Tanzania Shillings |
| **TV** | Television |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **USD** | United State Dollar |
| **UNDP** | United Nations Development Programme |
| **UNICEF** | United Nations Children's Fund |
| **UNESCO** | United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization |
| **UDSM** | University of Dar es Salaam |
| **ZAWA** | Zanzibar Water Authority |
| **ZBC** | Zanzibar Broadcasting Cooperation |
| **ZNZ** | Zanzibar |
| **ZLCR** | Zanzibar Law Resource Centre |
| **ZU** | Zanzibar University |

# HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA UTALII NA MAMBO YA KALE, MHESHIMIWA LELA MUHAMED MUSSA (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA, AKIWASILISHA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya njema na kuweza kutukutanisha tena katika Baraza lako ili tuweze kujadili mambo ya msingi ambayo yatachangia katika kuleta Maendeleo ya Nchi yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atusimamie katika kuitekeleza shughuli hii kwa imani, upendo na uwajibikaji.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwa idhini yako, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama Kamati ili ipokee, ijadili na hatimaye ikubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa udhati kabisa naomba kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa juhudi za makusudi anazozichukuwa katika kuiongoza nchi yetu pamoja na kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020- 2025. Utekelezaji wa Ilani hiyo umejikita zaidi katika kuwaletea Maendeleo makubwa Wananchi wa Visiwa vya Unguja na Pemba. Aidha, katika kipindi chake kifupi cha uongozi tumeshuhudia mabadiliko makubwa ya kiutendaji kwa Watumishi wa Umma jambo ambalo linachangia kupatikana kwa maendeleo

ya haraka. Vile vile, nimpongeze kwa jitihada zake alizozichukua za kuhakikisha kwamba Serikali atakayoiongoza ya awamu ya nane itafuata takwa la Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ya kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ambapo sote ni mashahidi kwamba Serikali hiyo sasa ipo na inafanya kazi kubwa ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kutudumishia Amani, Umoja na Upendo katika nchi yetu.

4. **Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kushika nafasi hiyo ya Urais, baada ya kifo cha aliyekua Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kilichotokea tarehe 17/3/2021, tunamuomba Mwenyezi Mungu aipumzishe kwa amani roho ya marehemu. Pia, niendelee kumpongeza mama Samia Suluhu Hassan kwa kuweka historia kuwa mwanamke wa kwanza kwa Tanzania kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia, kwa sasa ni mwanamke wa kwanza Tanzania kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amzidishie uwezo na ujasiri katika kulitumikia Taifa la Jamhuri ya Muungano Tanzania.

5. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, uteuzi huu umekuja baada ya kifo cha aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad aliyefariki tarehe 17/2/2021. Tunamuomba Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema Peponi, Amiin.

6. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, naomba kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa utendaji kazi uliotukuka anaouonesha wakati wa

kutekeleza majukumu yake pamoja na jitihada anazozifanya za kumsaidia na kumshauri vyema Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, katika kutekeleza majukumu ya kila siku.

7. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, napenda kukushukuru wewe binafsi na wasaidizi wako wote wakiwemo Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza, Katibu wa Baraza, Wajumbe wa Baraza, Maofisa na wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri zinazotekelezwa za kuliendeleza Baraza hili.

8. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii adhimu kuipongeza Kamati ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kilimo, Biashara na Utalii ikiongozwa na Mwenyekiti wake shupavu, Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Aza January Joseph pamoja na wajumbe wake wote kwa Maelekezo, Miongozo na ushauri makini wanaotupa wakati wa kutekeleza Majukumu na Miradi ya Maendeleo ya Wizara. Mimi binafsi na watendaji wenzangu wote tunafarijika sana kuwa nao pamoja na kushirikiana vizuri katika utekelezaji wa kazi zetu.

## B. MUUNDO WA WIZARA

9. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ina dhamana ya kusimamia Sekta Kuu mbili ambazo ni Utalii na Mambo ya Kale. Sekta hizi hujumuisha Kamisheni moja, Idara nne, Taasisi moja, Mamlaka moja na Ofisi Kuu Pemba ambazo ni: -

i. Kamisheni ya Utalii Zanzibar
ii. Idara ya Utalii
iii. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale
iv. Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa

v. Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe
vi. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
vii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
viii. Ofisi Kuu Pemba

## C. MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA

**10.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale pamoja na mambo mengine pia inatekeleza majukumu yafuatayo: -

i. Kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi.

ii. Kukuza pato la nchi kupitia Sekta ya Utalii.

iii. Kuwashawishi wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuanzisha miradi ya utalii itakayotoa tija kwa wananchi.

iv. Kuyalinda, kuyahifadhi na kuyatangaza maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini.

v. Kuvitunza vitu na mabaki ya kihistoria yaliyopo nchini ili kuweka kumbukumbu kwa faida ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

vi. Kuzilinda na kuzitunza nyaraka za Serikali kwa maslahi ya Taifa

vii. Kuuhifadhi na kuuendeleza Mji Mkongwe wa Zanzibar

## D. PROGRAMU KUU ZA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

**11.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inatekeleza Malengo na Majukumu kwa kufuata mfumo maalumu wa bajeti (Program Based Budget, PBB), ambapo Wizara inasimamia programu kuu tano na programu ndogo tano.

**Programu Kuu za Wizara ni : -**

i. Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii.
ii. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe.
iii. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii.
iv. Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii.
v. Programu ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

**Programu ndogo za Wizara ni: -**

i. Uendelezaji wa Makumbusho, Uhifadhi wa Mji Mkongwe na Mambo ya Kale.
ii. Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa
iii. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara.
iv. Utawala na Uendeshaji katika sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.
v. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba.

## E. UTALII NA UCHUMI WA BULUU

**12.** **Mheshimiwa Spika,** utalii wetu wa Zanzibar unakwenda sambamba na falsafa ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi ya "Uchumi wa Buluu" ambapo kupitia bahari tuliyojaaliwa na Mwenyezi Mungu itachangia kwa kiasi kikubwa shughuli na vivutio vya utalii nchini. Kwani nchi yetu ina bahari na fukwe nzuri ambazo watalii wengi duniani huvutiwa na uwepo wa vitu hivi. Kwa sasa, Wizara imepanga kutilia mkazo kuzitumia rasilimali za bahari kuwavutia watalii.

13. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wawekezaji wa sekta binafsi imelenga kuzitumia vizuri rasilimali za bahari kama matumbawe, samaki, visiwa vidogo vidogo pamoja na fukwe kwa kuvitangaza zaidi kwa wageni na wenyeji pamoja na kutoa fursa kwa wageni hao kutembelea rasilimali hizo. Pia, Wizara imepanga mikakati ya kushirikiana na sekta binafsi katika kuwekeza na kuimarisha michezo ya baharini na ufukweni ambayo ni kivutio kikubwa kwa watalii, kuwepo kwa shughuli hizi kutaongeza ajira kwa wananchi wetu pamoja na kukuza pato la nchi kupitia shughuli hii.

## F. MCHANGO WA SEKTA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KATIKA MAENDELEO YA NCHI

14. **Mheshimiwa Spika,** kiuchumi sekta ya Utalii inaendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya nchi kwa kuingiza fedha za kigeni, ambapo inakadiriwa zaidi ya asilimia 27 ya pato la nchi (GDP). Sekta ya Utalii imeweza kutoa ajira za moja kwa moja kwa wananchi wa Zanzibar zipatazo 33,000 na ajira zisizo za moja kwa moja zipatazo 72,000. Pia, kukua kwa Sekta ya Utalii kumepelekea hamasa kubwa kwa wananchi wa Zanzibar kujiwekeza katika shughuli za kilimo, uvuvi, ufugaji na usafirishaji, jambo ambalo asilimia kubwa ya mazao yao hutumika sana katika mahoteli na mikahawa ya wageni. Kuimarika kwa sekta ya Utalii kunasaidia sana shughuli za kiuchumi nchini mwetu kwa kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja pamoja na kuongeza pato la nchi.

15. **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar imebarikiwa kuwa na majengo na maeneo mengi ya kihistoria ambayo huipa sifa duniani kote. Kuendelea kubaki Mji Mkongwe wa Zanzibar katika Urithi wa

Dunia ni kielelzo tosha. Kwani wageni na watu wengi mashuhuri hutembelea Zanzibar kwa kuja kujionea Mji Mkongwe, pamoja na mabaki ya majengo ya kihistoria. Kwa kipindi kirefu majengo na maeneo hayo ya kihistoria hayajapewa kipaumbele katika kuyahifadhi na kuyaimarisha jambo ambalo limepelekea maeneo mengi kuchakaa na mengine kuanguka. Kwa sasa, Serikali imeweka Mkakati Maalumu wa kushirikiana na sekta binafsi kwa kuyaimarisha maeneo hayo ya kihistoria ili yazidi kuendelea kuwa kivutio kwa wageni na kuongeza idadi ya siku za ukaazi kwa wageni wanaoingia nchini.

## G. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

16. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ilikadiriwa kupata **shilingi 12,851,718,328/=** kwa ajili ya kutekeleza programu kuu tano na Miradi ya Maendeleo ya Wizara. Kati ya hizo **shilingi 8,151,718,328/=** kwa kazi za kawaida na **shilingi 4,700,000,000/=** kwa kazi za Maendeleo. Aidha, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya **shilingi 5,814,351,000/=** zinazokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali.

17. **Mheshimiwa Spika, j**umla ya **shilingi 4,259,102,898/=** zilipatikana kwa kazi za kawaida sawa na **asilimia 52.25**, kwa upande wa kazi za miradi ya maendeleo zimepatikana **shilingi 1,357,250,612.69** sawa na **asilimia 28.88**. Aidha, Wizara ilikusanya **shilingi 3,332,804,202/=** sawa na **asilimia 57.32** zilizoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1A hadi 1C).**

## H. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

18. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara imefanikiwa kutekeleza miradi ifuatayo: -

**Programu ya Kuimarisha na Kuendeleza Maeneo ya Kihistoria**

19. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ilipanga kuyaimarisha maeneo ya kihistoria kwa kufanya matengenezo Makumbusho ya Viumbe Hai na Makumbusho ya Amani yaliyopo Mnazi Mmoja Unguja, kuimarisha pango la Watoro na pango la Kijiji yaliyopo Makangale Pemba, kuimarisha Miskiti na Makaburi ya kihistoria yaliyopo Chwaka Tumbe.

20. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeamua kuzipitia na kuzihakiki zabuni za miradi zilizotumika kwa ajili ya kuwapata wakandarasi waliotarajiwa kuyafanyia matengenezo maeneo ya kihistoria kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Lengo la kuzipitia zabuni hizo ni kupata thamani halisi ya fedha (Value for Money) itakayotumika katika utekelezaji wa miradi. Ripoti ya tathmini ya miradi mipya ya mwaka 2020/2021 zilipitiwa na ikagundulika yapo mapungufu yangeigharimu Serikali zaidi ya **Shilingi 500,000,000/=.** Hivyo, Wizara imerudia tena utaratibu wa manunuzi na unategemewa kukamilika utaratibu huo mwishoni mwa mwezi Mei, ambapo wajenzi wapya watakua washapatikana.

21. **Mheshimiwa Spika,** kwa miradi inayoendekea, Wizara imekamilisha zoezi la tathmini ya miradi. Uchunguzi wa awali

umegundua upunngfu mkubwa kwenye mradi wa Mkama Ndume Pemba**,** ambapo Kamati ya Tathmini imependekeza kurudia kwa mazungumzo na Mkandarasi kabla hatujakamilisha malipo ya mwisho.

**22.** **Mheshimiwa Spika,** napenda kukuarifu kwamba katika kipindi hichi Wizara ilikuwa ikiendelea na utekelezaji wa miradi iliyoanza utekelezaji wake mwaka wa fedha 2019/2020, miradi hiyo ni kuimarisha nyumba ya kihistoria ya Wareno iliyopo Mvuleni Unguja, kuimarisha nyumba ya Mtawala ya Jadi Mwinyi Mkuu iliyopo Dunga Unguja pamoja na kuimarisha eneo la kihistoria la Mkamandume liliyopo Pujini Pemba. Hata hivyo, Wizara itaanza kufanya thathmini halisi ya miradi 'value for money' kabla hatujamalizia malipo ya Wakandarasi ili kuhakikisha kuwa thamani za miradi zinaendana na gharama za miradi hio kwa mujibu ya Sheria.

**23.** **Mheshimiwa Spika,** eneo la Kihistoria la Mvuleni linajengwa na Kampuni ya **KIN INVESTMENT LTD,** mradi huu umetengewa jumla ya **Tsh 695,855,383/=** hadi kufikia Machi 2021 mjenzi ameshalipwa **Tsh 487,725,845.76/=** sawa na **asilimia 70**, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 80**. Mradi huu umeanza tarehe 28/11/2019 na unategemewa kukamilika tarehe 31/5/2021.

**24.** **Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa kuliimarisha eneo la kihistoria la Mwinyi Mkuu kwa awamu ya pili unatekelezwa na Kampuni ya **YASIN & SONS COMPANY LTD**. Mradi huu umetengewa jumla ya **Tsh 802,474,304.60/=** hadi kufikia Machi 2021 mjenzi tayari ameshalipwa **Tsh 550,154,747.83 /=** sawa na **asilimia 69**, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 93**. Mradi huu umeanza tarehe 15/11/2019 na unategemewa kukamilika tarehe 31/5/2021.

**25.** **Mheshimiwa Spika,** mradi wa Kuliimarisha eneo la Kihistoria la Mkamandume Pemba kwa awamu ya pili unatekelezwa na Kampuni ya **SHAMJO COMPANY LTD.** Mradi huu umetengewa jumla ya **Tsh 878,309,587.00/=** hadi kufikia Machi 2021 mjenzi ameshalipwa **Tsh 594,211,856.95/=** sawa na **asilimia 68**, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 90**. Mradi huu umeanza tarehe 23/12/2019 na unategemewa kukamilika tarehe 31/5/2021.

**Ukarabati wa jengo la Beit-El-Ajaib**

**26.** **Mheshimiwa Spika,** jengo mashuhuri la daraja la kwanza la Beit El Ajaib liliporomoka sehemu yenye wastani wa asilima 20 ya jengo zima katika upande wa Kaskazini-Magharibi mnamo tarehe 25 Disemba, 2020. Hitilafu hiyo ilipoteza maisha ya mafundi wawili na majeruhi wanne pamoja na kuathiri jengo ambalo ni sura na haiba ya Zanzibar, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa kupitia Baraza lako ninachukuwa fursa hii kutoa salamu za pole kwa familia zote zilizoathirika na janga hili.

**27.** **Mheshimiwa Spika,** kufuatia kadhia hii Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, alikutana na Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) nchini Tanzania Bw. Tirso Dos Santos Ikulu mjini Zanzibar mwanzoni mwa mwezi wa Januari, 2021. Kufuatia kikao hicho cha Mhe. Rais, UNESCO waliomba kuleta wataalamu nchini kwa kuisadia Serikali katika utekelezaji bora wa ukarabati wa jengo la Beit El Ajaib.

**28.** **Mheshimiwa Spika,** tayari timu mbili za wataalamu kutoka UNESCO ziliwasili Zanzibar, timu ya awali ilianza kwa kurekodi hali halisi ya jengo katika teknolojia ya “3D” na timu ya pili

iliendelea kufanya uchunguzi wa kiuhandisi ya jengo la Beit al ajaib kwa kutumia matokeo ya timu ya awali, matokeo ya timu mbili hizi zimeshawasilishwa Kituo cha Urithi wa Kimataifa cha UNESCO mwanzoni mwa mwezi wa Machi, 2021, ambao na wao tayari wameshawasilisha ripoti hizo Serikalini. Taarifa za ripoti zote mbili zimeishauri Serikali kabla ya kuendelea na ujenzi wa jengo hilo kufanya uchunguzi wa kitaalamu katika udongo (Geotechnical investigation) na kuchunguza umazubuti wa mihimili ya jengo (Structural analysis) ili kujua njia bora ya kuendelea na ujenzi wake. Vile vile, zimeshauri hatua zaidi za kulihami jengo ziendelee kuchukuliwa ili kuweka mazingira salama kwa jengo lenyewe.

29. **Mheshimiwa Spika,** kwa sasa, Wizara inaufanyia kazi ushauri wa UNESCO kwa kufanya utafiti wa jengo na udongo wa Beit el Ajaaib. Aidha, Wizara inaendelea kulihami jengo kwa kuweka miunda katika sehemu zote zilizo wazi na kuziba nyufa zinazopitisha maji ambazo zinahatarisha usalama wa jengo. Mara baada ya kukamilika kwa tafiti hizi, taratibu za kutangaza tenda kwa ajili ya ujenzi wa jengo hili zitaanza ambapo Serikali ya Oman wameahidi kuendelea na ufadhili wa ujenzi huo.

**Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii**

30. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inatekeleza Mradi wa kuimarisha utalii kwa wote ambapo katika mwaka wa fedha 2020/2021 mradi huu umetengewa **shilingi 2,000,000,000/=**. Wizara tayari imekamilisha taratibu zote za manunuzi na kuipata Kampuni ya **KIN INVESTMENT COMPANY LTD**, ambayo ndio itakayofanya kazi ya kuliendeleza eneo la Bungi kwa awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huu.

## I. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

31. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ilipanga kutekeleza programu kuu nne kama ifuatavyo: -

i. Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii.

ii. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe.

iii. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii.

iv. Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii.

v. Programu ya Utawala na Uendeshaji katika sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

## I. PROGRAMU YA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII.

32. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuratibu na kusimamia shughuli za Utalii nchini, matokeo ya muda mrefu ni kuwa na utalii endelevu na wenye tija kwa maslahi ya nchi na wananchi, huduma zinazotolewa katika programu hii ni kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na mipango ya utalii. Programu hii inatekelezwa na Idara ya Utalii.

**UTEKELEZAJI HALISI**

33. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Utalii kwa kushirikiana na Idara ya Kilimo imefanya mikutano na wamiliki wa mashamba ya viungo ya Kidichi, Dole na Kizimbani kwa ajili ya kujadili namna ya kuyaimarisha mashamba hayo. Wamiliki wa mashamba wamepatiwa elimu ya kuyaimarisha mashamba ili yaweze kutoa huduma nzuri kwa watalii. Aidha, watoa maelezo (Tour guide) kwenye mashamba

ya viungo wamepewa elimu kuhusu kazi, faida na aina ya viungo na miti inayopatikana katika mashamba ya viungo. Pia, Idara imetoa elimu ya mashamba ya viungo yaliyopo Mtape na shamba la Mtakata Pemba juu ya uimarishaji wa mazao ya viungo nchini.

34. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Utalii imeshirikiana na Jumuiya ya Maendeleo ya Muungoni, iliyopo Mkoa wa Kusini Unguja na kuweza kuibua maeneo mapya ya vivutio vya utalii, vikiwemo sehemu iliyoanguka ndege ya jeshi ya vita vya pili vya dunia (Duta), mskiti wa kale, mabaki ya soko la kale, mkwaju wa kale, kisiwa ndege, mwembe uganga, bandari ya kale, pango la makasi, mzimu wa mama yaya, na mji wa kale. Kwa sasa maeneo haya yapo katika hatua ya kuendelezwa ili yaweze kutembelewa na watalii wanaoingia nchini.

35. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Utalii imefanya vipindi vitatu katika televisheni ya ISLAND TV na kuzungumza na wananchi juu ya faida na changamoto katika sekta ya utalii na kuwaelekeza wananchi wanaojishughulisha katika sekta ya utalii njia bora za kujikinga na maradhi ya corona. Aidha, Idara imefanya kipindi kimoja katika redio jamii Mkoani FM juu ya nafasi ya utalii kiuchumi na kimazingira.

36. **Mheshimiwa Spika,** Idara kwa kushirikiana na LEO (Labour Empowerment Organization) na taasisi za Serikali na wadau wa utalii, ilifanya usafi katika kisiwa cha Kwale kwenye maeneo ya utalii. Pia, Idara iliendelea na usafi katika Wilaya ya Kaskazini “A” kwa maeneo ya Nungwi na Kiwengwa. Aidha, Idara imeshirikiana na Wilaya zote za Unguja wameandaa Mpango Maalumu wa Usafi katika maeneo yote ya utalii yaliyopo nchini. Lengo la kampeni hii ni kuweka mazingira na mandhari nzuri ya vivutio vyetu vya utalii.

37. **Mheshimiwa Spika,** Idara imesimamia marekebisho ya Sheria ya Utalii nambari 6 ya mwaka 2009, pamoja na marekebisho yake ya Sheria ya utalii nambari 7 ya mwaka 2012. Rasimu ya Sheria hii imewasilishwa kwa wadau na kwa sasa inajadiliwa na wajumbe wa Kamati Tendaji ya Wizara kabla ya kuwasilishwa kwa Tume ya Kurekebisha Sheria.

38. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi **228,149,700/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2021 imefanikiwa kupata shilingi **141,313,550/=** sawa na **asilimia 61.94**. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D)**.

## II. PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE.

39. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii kuwa na Mji Mkongwe na maeneo ya kihistoria yaliyohifadhiwa, kuimarishwa na kuendelezwa kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadae pamoja na kutumia njia za kisasa katika uhifadhi wa Nyaraka na kumbukumbu za Serikali, matokeo ya muda mrefu ni kuzitunza nyaraka na kumbukumbu za Serikali pamoja na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria na Uhifadhi wa Mji Mkongwe ili kubakia kuwa urithi wa kitaifa na kimataifa kwa kuyahifadhi kuyalinda na kuyatangaza. Programu hii imeundwa na programu ndogo mbili ambazo ni: -

i. Uendelezaji wa Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe
ii. Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa

**Progaramu Ndogo: Uendelezaji wa Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe**

40. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Uendelezaji wa Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe inatekelezwa na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe.

41. **Mheshimiwa Spika,** huduma zinazotolewa na programu hii ni Uhifadhi na Uendelezaji wa Makumbusho, Maeneo ya Kihistoria, Mambo ya Kale pamoja na Mji Mkongwe.

**UTEKELEZAJI HALISI**

42. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imekabidhiwa rasmi lililokuwa jengo la Ofisi za Wareno ambalo limefanyiwa matengenezo makubwa na kampuni ya **KIN INVESTMENT LTD** liliopo Fukuchani Unguja, matengenezo hayo yaligharimu **Tsh 320,542,870/=.** Matengenezo hayo yalijumuisha ukarabati wa jengo lote la kihistoria pamoja na kujenga jengo jipya la kutolea huduma (Service Building) kwa wageni watakaofika eneo hili. Kufanyiwa matengenezo jengo hili kunaongeza idadi ya ajira kwa wananchi, idadi ya vivutio vya wageni vilivyopo nchini na kuchangia kukuza pato la nchi.

43. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua ya kuyalinda maeneo ya kihistoria Idara imefanikiwa kupata hati miliki katika maeneo ya Nyumba ya Wananchi Forodhani (Palace Museum), Ngome Kongwe, Hamamu ya Hamamni, Makumbusho ya Mnazi Mmoja na Nyumba ya Beit el Ajaab Forodhani. Kupatikana kwa hatimiliki hizi kunapelekea kwa

sasa Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale kuwa na hatimiliki 19 kati ya maeneo ya kihistoria 86 yaliyotangazwa rasmi katika gazeti la Serikali.

44. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imefanya utafiti katika eneo la kihistoria la Mkumbuu Pemba kuhusu historia ya eneo hilo na tayari ripoti ya utafiti huo imekamilika. Aidha, Idara imefanya utafiti mdogo kwa maeneo ya Mkokotoni ya Shangani, Chemchem na kwa Mazinge Unguja kwa ajili ya kupata historia ya eneo hilo. Kufanyika kwa tafiti hizi kunaisaidia Idara kuweza kuyatambua na kuyaibua maeneo mapya ya kihistoria ambayo yatachangia kuwa vivutio vya utalii vilivyopo nchini. Pia, Idara imeandaa na kuweka mabango ya maelezo katika maeneo ya kihistoria ya Bungi, Mvuleni, Mtoni na Maruhubi ili kutoa historia fupi ya kila eneo husika.

45. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua ya kuyatangaza maeneo ya kihistoria kwa wananchi ili waweze kuyatambua zaidi Idara imeratibu ziara kwa waandishi wa habari wa ZBC Radio na TV, Chuchu FM, Hits FM, Habari FM, Alfalah KTV online, NTV online, Habari Maelezo na Zenj TV wakishirikiana na wafanyakazi wa Idara ya Makumbusho katika maeneo ya kihistoria ya Kizimkazi Msikiti wa Kale, Pango la Miza wa Miza na Pete. Aidha, Idara imekutana na wadau wa Mambo ya Kale kwa lengo la kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuyalinda na kuyahifadhi maeneo ya kihistoria pamoja na kushirikiana nao katika hatua ya kuyatangaza maeneo hayo. Vile vile, Idara imechapisha na kusambaza vipeperushi 500 vya maeneo ya kihistoria kwa watembeza watalii ili kuyatangaza maeneo hayo.

46. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imeshiriki katika maonesho ya biashara katika viwanja vya Maisara ya kuadhimisha miaka 57 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar pamoja na kushiriki katika maonesho ya nane nane yaliyofanyika Kizimbani Unguja. Aidha, Idara imetayarisha na kurusha hewani jumla ya vipindi 18, ambapo vipindi viwili ZBC TV, vipindi vinne Zanzibar Cable, vipindi vinne Chuchu FM, vipindi vinne Hits FM na vipindi vinne Haiba TV. Lengo la shughuli hii ni kujitangaza zaidi kwa wananchi na wadau wa utalii.

47. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale ilipokea jumla ya Wageni 4,643 waliotembelea maeneo ya kihistoria ndani ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Kati ya Wageni hao Wenyeji ni 626 na Wageni kutoka Mataifa ya nje 1529. Pia, Wageni Maalumu walikuwa ni 16 na idadi ya Wanafunzi ni 2,472.

48. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe ina jukumu la kuhakikisha kwamba urithi wa kihistoria wa majengo, utamaduni wa asili, mandhari, na vivutio vyengine vya Mji Mkongwe vinabakia katika hali yake ya asili kwa faida ya vizazi vya sasa na vizazi vijavyo pamoja na kudumisha hadhi ya urithi ya mji wetu duniani.

49. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021 Mamlaka imeendelea kusimamia uhifadhi na uendelezaji wa Mji wetu wa Urithi wa Kimataifa kwa kufanya kazi zifuatazo: -

50. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ilisimamia kazi za ukarabati na ujenzi mpya wa jengo lililokuwa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) liliopo Malindi, ambapo Mamlaka ilihakikisha kwamba umefuata na kuzingatia ramani zilizopasishwa, kazi zote za ujezi na ukarabati

zimeshakamilika na jengo limeshakabidhiwa kwa wamiliki. Aidha, Mamlaka imetoa jumla ya vibali 125 kwa matengenezo ya kawaida kwa nyumba mbali mbali zilizomo ndani ya eneo la uhifadhi. Pia, Mamlaka hufanya ufuatiliaji ili kuhakikisha kwamba waliopatiwa vibali hivyo hawakiuki masharti ya ruhusa walizopatiwa.

**51.** **Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchakavu wa Majengo Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe ilifanya kikao na wamiliki wa majengo ya Mji Mkongwe wakiwemo Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Shirika la Nyumba la Zanzibar kwa ajili ya kutayarisha ripoti ya tathmini ya hali ya majengo wanayoyamiliki. Jumla ya majengo 127 yamebainika kua katika hali mbaya, aidha Mamlaka inaendelea kuchukua jitihada za kuwajuilisha wamiliki wa majengo kuchukua hatua za kuyafanyia matengenezo majengo yao kila inapohitajika ili kuepusha madhara yanayoweza kusabishwa na uchakavu wa majengo yao. **(Tafadhali angalia kiambatisho nambari 3)**

**52.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka kwa kushirikiana na Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) imetayarisha kipindi Maalumu kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na Uhifadhi wa Mji Mkongwe, kipindi hicho kinafahamika kwa jina la Mkono kwa Mkono na kinarushwa moja kwa moja kila siku ya Alkhamis saa moja kamili za usiku. Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na Jumuiya ya uhifadhi wa Mji Mkongwe imetoa mafunzo kwa wafanyabiashara 56 wa masoko yaliyomo ndani ya eneo la uhifadhi wa Mji Mkongwe juu ya umuhimu wa kuuhifadhi na kuulinda urithi pamoja na mazingira yanayozunguka maeneo hayo.

**53.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imefanya safari tano za kikazi ambazo zilihusisha ukaguzi wa jengo la kihistoria linalojulikana

kwa jina la Caravan-Serai liliopo Bagamoyo kwa ajili ya kulifanyia makisio ya ukarabati, kujadili ripoti za hali ya uhifadhi kwa miji ya urithi-Arusha, kuhudhuria mkutano kwa mameneja wa maeneo ya urithi, kuutambulisha uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kamisheni ya UNESCO pamoja na uandaaji wa mihutasari ya somo la historia, vikao hivi vilifanyika katika Mji wa Dar-es Salam. Aidha, Mamlaka imefanya vikao vinne vya bodi ya Wakurugenzi na vinne vya zabuni ili kujadili masuala mbali mbali yanayohusiana na uendeshaji wa ofisi.

**54.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 1,994,397,598/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2021 imefanikiwa kupata **shilingi 1,201,428,882/=** sawa na **asilimia 60**. Aidha, shilingi **2,700.000.000/=** kwa ajili ya kazi za maendeleo hadi kufikia Machi 2021 **shilingi 1,004,996,904.69/=** sawa na **asilimia 37.22** zimepatikana. Pia, Programu ndogo hii imetakiwa kukusanya jumla ya **shilingi 275,031,000/=** hadi kufikia Machi 2021, jumla ya **shilingi 106,019,474/=** zimekusanywa sawa na **asilimia 38.55**. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D na 1E).**

## Programu Ndogo: Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa

**55.** **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa inatekelezwa na Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa.

**56.** **Mheshimiwa Spika,** huduma zinazotolewa na programu ndogo hii ni Kuhifadhi na Kusimamia Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa kwa matumizi ya Serikali na matumizi ya Umma.

**57.** **Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu imefanya ukaguzi wa kumbukumbu katika Wizara 15 za Unguja na Pemba na kupatiwa ushauri na maelekezo ya utunzaji na uhifadhi bora wa kumbukumbu hizo ili ziweze kuleta tija kwa Taifa. Pia, Taasisi ya Nyaraka imeendesha zoezi maalumu la kuondosha baadhi ya majalada kwa Taasisi za Serikali na kuyaweka katika mfumo mzuri, ambapo kutowekewa utaratibu wa kuhifadhiwa vyema majalada hayo kunapelekea baadhi ya majalada yenye taarifa muhimu za Serikali kupotea.

**58.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuzilinda na kuzihifadhi nyaraka za nchi, Taasisi ya Nyaraka imefanikiwa kuyahifadhi jumla ya majalada 7,594 (sawa na Folios 240,780) kwenye mfumo wa ki-elektroniki. Aidha, Taasisi ya Nyaraka imetoa huduma za utafiti kwa watafiti 156 wakiwemo wageni wawili kutoka nchi ya Marekani na Urusi pamoja na wenyeji 154. Pia, Taasisi imepokea wanafunzi 162 kutoka Vyuo mbali mbali walifika Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu kwa kujifunza kwa vitendo (Field Attachments) njia bora za uhifadhi wa kumbukumbu.

**59.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 668,202,460 /=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2021 imefanikiwa kupata **shilingi 405,178,752/=** sawa na **asilimia 60.64**. Pia, Programu ndogo hii imetakiwa kukusanya jumla ya **shilingi 7,094,000/=,** hadi kufikia Machi 2021, jumla ya **shilingi 116,150/=** zimekusanywa sawa na **asilimia 1.64**. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D na 1E)**.

## III. PROGRAMU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI UTALII

60. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuongeza uelewa kwa wakazi wa Tanzania na jamii ya kimataifa kuhusu bidhaa na huduma za utalii zilizopo Zanzibar. Programu inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi.

61. **Mheshimiwa Spika,** huduma inayotolewa katika programu hii ni kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi ili Zanzibar itambulike zaidi kuwa ni kituo bora cha utalii duniani.

**UTEKELEZAJI HALISI**

62. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya utalii imeendelea kuhamasisha utalii wa ndani kwa kushirikiana na wadau kupitia Maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Saba saba) - Dar es Salaam; Maonesho ya Kilimo Nanenane -Kizimbani, Maonesho ya Siku ya Chakula Duniani - Chamanangwe, na Maonesho ya Biashara - Maisara katika kuadhimisha miaka 57 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Pilipili Family Hotels waliandaa Tamasha la Michezo lililopewa jina la Jambiani "Beach Soccer and Sport Tourism Festival" ambalo limefanyika Jambiani likijumuisha michezo ya mpira wa ufukweni (beach soccer), resi za ngalawa, resi za baskeli, resi za Kukimbia kwa miguu (Marathon) na kuvuta kamba. kushiriki katika matamasha haya kunahamasisha dhana ya utalii kwa wote kwani wananchi wengi wanapata fursa ya kushiriki kwa njia moja au nyengine.

63. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni imeandaa "Farm Trip" kwa timu za mpira wa miguu zilizoshiriki Mapinduzi Cup timu hizo ni Simba,

Yanga, Azam na Mtibwa pamoja na kumualika mwanamuziki maarufu nchini Zuhura Othman Maulid (Zuchu) kutembelea vivutio vya utalii mbali mbali kama vile Jozani, Mji Mkongwe, Mnarani Aquarium kwa lengo la kuvitangaza ndani na nje ya nchi kwa njia za televisheni na mitandao ya kijamii.

**64.** **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii imeendelea kushajihisha utalii kupitia vyombo vya habari vya Redio na Televisheni. Jumla ya vipindi 74 kupitia ZBC redio vipindi 22, ZBC TV vipindi vinane, Zanzibar Cable TV vipindi vitano, Chuchu FM vipindi 20, Bahari FM vipindi 11, Redio Jamii ya Micheweni vipindi vinne na Sauti ya Jamii Chokocho vipindi vinne.

**65.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi, Kamisheni ya Utalii imetangaza vivutio vya utalii vilivyopo Zanzibar kwa njia ya picha "virtual" na kufanya mikutano kwa njia ya mitandao "zoom meeting" kutokana na kuendelea kwa janga la maradhi ya Corona duniani. Mikutano hiyo ni pamoja na shirika la ndege la KLM, Giant Tour Operator ya Marekani, Tanzania Qatar Business Forum na Russia Tanzania Cultural Center. Mazungumzo hayo yamepelekea kupata ongezeko la wageni kutoka soko la Ulaya Mashariki la Urusi, Ukrain na Poland. Katika kipindi cha Januari hadi Februari 2021, Zanzibar imepokea wageni 56,496 kutoka mataifa ya Ulaya Mashariki, ukilinganisha na kipindi kama hicho kwa nchi hizo kwa mwaka 2020 Zanzibar ilipokea wageni 12,812.

**66.** **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii imeratibu safari ya waandishi wa habari 18 ambapo waandishi watano wanatoka Kampuni ya 24 Travel Channel ya Urusi, waandishi wanne wanatoka Kampuni ya Russian TV, waandishi sita kutoka Nile TV International

ya Misri na waandishi watatu kutoka kampuni ya Botravail ya nchini Ufaransa. Waandishi hawa wametengeneza filamu kutoka kwenye vivutio vya utalii na kuzionesha filamu hizo kwenye televisheni za nchi zao ili kuongeza idadi ya wageni wanaotembelea Zanzibar. Kupitia waandishi hawa Zanzibar imepata fursa ya kutangazwa katika nchi hizo kupitia vyombo hivi vya habari kwa gharama nafuu.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021 program hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi **602,830,000/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2021 imefanikiwa kupata shiling **99,437,250/**= sawa na **asilimia 16**. (**Tafadhali angalia kiambatisho nambari 1D).**

## IV. KURATIBU NA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII

6**8.** **Mheshimiwa Spika,** lengo la programu hii ni kuongeza tija ya sekta ya Utalii na kuweka mazingira na rasilimali watu bora katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya Utalii. Programu hii inatekelezwa na Idara ya Mipango na Sera katika Kamisheni ya Utalii na malengo yake makuu ni kuweka mazingira na rasilimali watu bora katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya Utalii.

### UTEKELEZAJI HALISI

**69.** **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii imeendelea kufanya ukaguzi wa miradi ya biashara za utalii ili kubaini wanaofanya biashara kinyume cha Sheria ya Utalii. Kazi hiyo imefanyika katika mikoa yote ya Zanzibar. Aidha, kazi hiyo pia imetekelezwa kwenye vivutio vya utalii kama vile Jozani na Mashamba ya viungo ya

Kizimbani na Dole. Katika ukaguzi huo, jumla ya miradi ya utalii 1,400 imekaguliwa. Miradi hiyo imejumuisha hoteli, mikahawa, michezo ya baharini na kampuni za kuandaa misafara ya watalii. Pamoja na mambo mengine ukaguzi huo pia uliangalia mambo mbali mbali kama vile idadi ya vyumba na wafanyakazi, huduma zinazotolewa pamoja na kutoa ushauri wa uendeshaji bora wa biashara zao.

70. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii imeendelea kuwahamasisha Wazanzibar kuwekeza katika sekta ya utalii ikiwa ni utekelezaji wa dhana ya utalii kwa wote. Kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 jumla ya miradi ya wazawa 60 imeanzishwa ikiwemo nyumba za kulaza wageni, Kampuni za kuandaa misafara ya watalii, mikahawa na Kampuni za michezo ya baharini. Miradi hii imechangia kwa kiasi kikubwa ajira kwa vijana wetu wa Zanzibar.

71. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha Utalii katika kisiwa cha Pemba, Kamisheni imeendesha mafunzo ya utalii kwa Wajasiriamali 45 kutoka Wilaya ya Wete, Mkoani, Chakechake na Micheweni. Lengo la mafunzo hayo ni kuwaelimisha namna bora ya kutoa huduma za utalii kwa wateja wao. Adha, katika kuhakikisha kuwa mazingira ya kufanyia kazi yanaimarishwa ili kuongeza ufanisi katika kazi na utoaji huduma bora kwa wananchi, Kamisheni ya Utalii imewasomesha wafanyakazi wake watatu katika vyuo vya ndani ya nchi katika fani za utalii na manejimenti ya miradi (Project Management).

72. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha upatikanaji wa taarifa za kutosha za watalii wanapoingia nchini Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Maliasili na Utalii ya Tanzania Bara, Idara ya Uhamiaji na Ofisi ya Taifa ya Takwimu

wanaendelea na utafiti (Exit survey) ambao uko katika hatua ya uchambuzi wa taarifa. Kukamilika kwa utafiti huo kutapelekea kufahamu baadhi ya viashiria muhimu vya upimaji wa ukuaji wa sekta ya utalii ikiwemo matumizi ya mtalii kwa siku pamoja na siku zao za ukazi. Matokeo kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2020 siku za ukaazi kwa mgeni ni wastani wa siku saba. Kadhalika, mapato yanayoingia ndani ya uchumi wa Zanzibar (Tourism Earnings) ni dola za Kimarekani 380.1 milioni.

73. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na UNDP inatekeleza mradi ya uhuishaji wa sekta ya utalii baada ya kuathiriwa na maradhi ya Corona. Mradi huu unakusudia kuimarisha utangazaji wa huduma za utalii, kujenga uwezo kwa wadau wa utalii kwa kuwapatia mikopo na mafunzo, kuhakikisha huduma za utalii zinatolewa kwa kuzingatia uwepo wa maradhi ya Corona na kuhifadhi mazingira. Kupitia mradi huo vifaa mbali mbali vya utangazaji utalii vimenunuliwa ikiwemo vifaa kwa ajili ya mikutano ya mitandao (zoom meeting). Kupatikana kwa vifaa hivyo kumeongeza kasi ya utangazaji utalii. Kupitia mradi huo jumla dola za kimarekani 50,000 zimetolewa kwa wajasiriamali wa utalii. Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imefanya ukaguzi wa miradi ya utalii kwa lengo la kuangalia utekelezaji wa mwongozo wa utoaji wa huduma za utalii kwa kipindi cha Corona.

74. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango inaendelea na kazi ya kuandaa mfumo wa kielektroniki kwa lengo la kudhibiti upotevu wa mapato katika sekta ya utalii. Kupitia mfumo huo vifaa maalumu vitawekwa katika maeneo ya vivutio vya utalii na maeneo mengine kadri itakavyoonekana inafaa. Mfumo huu ambao unatarajiwa kuunganishwa na huduma za upatikanaji wa viza za kuingia Tanzania, unaandaliwa kwa

umakini bila ya kuathiri maendeleo ya sekta nchini na uendeshaji wa biashara ya utalii duniani kwa mfano uwepo wa booking.com, expedia na kadhalika. Kukamilika kwa mfumo huu kutawezesha Zanzibar kupata kodi halisi kutoka sekta ya utalii, kudhibiti nyumba za kulaza wageni zisizokuwa rasmi (Airbnb), kupata takwimu za utalii za uhakika kwa wakati pamoja na kujua mwenendo na taarifa za watalii wakati wote wanapokuwa nchini.

**75.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021 programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 1,512,470,000/-** kwa kazi za kawaida pamoja na **shilingi 2,000,000,000/=** kwa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2021 programu hii imefanikiwa kupata **shilingi 1,133,289,093/=** sawa na **asilimia 32** na kutakiwa kukusanya jumla ya **shilingi 5,492,029,000/=** na hadi kufikia Machi 2021 jumla ya **shilingi 3,226,297,078/-** zimekusanywa sawa na **asilimia 59**. Fedha hizi zinaingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D na 1E).**

## V. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

**76.** **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti pamoja na usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu katika Wizara. Programu hii imeundwa na programu ndogo tatu ambazo ni:

i. Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Utalii na Mambo ya Kale
ii. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara
iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba

**Programu Ndogo: Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Utalii na Mambo ya Kale**

**77.** **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Utalii na Mambo ya Kale inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

**78.** **Mheshimiwa Spika,** huduma zinazotolewa katika programu ndogo ni kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi, utayarishaji wa ripoti za fedha na ukaguzi pamoja na mpango wa manunuzi.

**UTEKELEZAJI HALISI**

**79.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi imesimamia ufanyaji wa tathmini ya utendaji kazi wa wafanyakazi wake 481 Unguja na Pemba na kujiridhisha na utendaji wao na kuwaombea nyongeza ya mwaka. Vilevile, Viongozi wa Wizara waliweza kufuatilia utendaji kazi Pemba. Pia, Idara imeratibu vikao 42 vya Kamati Tendaji na Kamati ya Uongozi ya Wizara kwa ajili ya kujadili Sera, kanuni, Sheria, Miongozo na Miradi mbali mbali ya maendeleo ya Wizara.

**80.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi imefanikiwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wake 15 katika fani na ngazi tofauti. **(Tafadhali Angalia Kiambatanisho nambari 2)**. Aidha, wafanyakazi 177 wamepatiwa mafunzo ya ndani juu ya uandaaji wa Mpango wa rasilimali Watu, Uandaaji wa Bajeti, Utayarishaji wa Mkataba wa huduma kwa umma na njia za kisasa za utoaji wa habari za Wizara ikiwemo kwa utumiaji wa mitandao ya kijamii.

81. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mashirikiano baina ya Wizara, Taasisi na Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa, Wizara imefanya jumla ya vikao 18 na Wadau wa Utalii na Mambo ya Kale wa ndani na nje ya nchi na kujadili maendeleo ya sekta. Wizara pia, imepokea wageni 12 kutoka mataifa mbali mbali na Mashirika ya Kimataifa kwa lengo la kuimarisha uhusiano mwema na mashirikiano ya utekelezaji wa shughuli za Wizara. Nchi hizo ni Oman, China Kenya na Mashirika ni pamoja na UNESCO, UNDP, UNICEF.

82. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 1,947,733,970/=** kwa kazi za kawaida, hadi kufikia Machi 2021 imefanikiwa kupata **shilingi 975,167,335/=** sawa na **asilimia 50.07**. **(Tafadhali angalia kiambatanisho nambari 1D).**

**Programu Ndogo: Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara**

83. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya kuratibu na kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la kupanga, kutayarisha, kufuatilia na kutathmini mipango, sera, tafiti na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

84. **Mheshimiwa Spika,** huduma ambazo zinatolewa ni uratibu wa sera na tafiti, kuandaa na kuwasilisha bajeti ya Wizara, kuandaa na kusimamia mipango na miradi ya maendeleo ya Wizara.

## UTEKELEZAJI HALISI

**85.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanya utafiti wa "Usahihi wa Taarifa katika Maeneo ya Kihistoria" tayari watafiti wameshakusanya taarifa za utafiti huo kwa upande wa Unguja na Pemba. Utafiti huu umelenga zaidi kuandika historia ya majengo na maeneo ambayo yalikuwa yakitumika baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964. Kazi hii imekuja baada ya kukamilika kazi ya awali kama hii ambayo illilenga kuyatafiti majengo na maeneo yaliyokuwa yakitumika kabla ya Mapiduzi ya mwaka 1964. Vitabu hivi vitasaidia sana kutunza historia kwa kizazi cha sasa na cha baadae, pia, vitabu hivi vitatumiwa na watembeza watalii (Tour Guide) kwani vinaelezea historia kwa majengo ya kale.

**86.** **Mheshimiwa Spika,** katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya Wizara kwa upande wa Pemba na Unguja, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefuatilia utekelezaji wa mradi inayotekelezwa Pemba ambayo ni uimarishaji wa eneo la kihistoria la Mkamandume kwa awamu ya pili pamoja na kuwakaguza Wajenzi katika miradi waliyoomba kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ambayo ni Kuiimarisha Misikiti na Makaburi ya Chwaka Tumbe na Kuiimarisha pango la Watoro na pango la Wanakijiji Makangale. Kwa upande wa Unguja miradi iliyofuatiwa Uimarishaji wa eneo la kihistoria la Mvuleni, Uimarishaji wa Kasri ya Mwinyi Mkuu pamoja na mradi wa Utalii kwa Wote uliopo Bungi. Aidha, Idara imewakaguza wajenzi katika miradi waliyoomba kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Unguja ambayo ni Uimarishaji wa Makumbusho ya Viumbe Hai na Makumbusho ya Amani yaliyopo Mnazi Mmoja.

**87.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeratibu na kusimamia mikutano ya wadau wa Utalii na Mambo ya Kale kwa

Unguja na Pemba, ambapo wadau wa sekta hizi wamepata fursa ya kukutana na uongozi wa Wizara. Katika mikutano hiyo mambo mbali mbali yalijadiliwa ikiwemo fursa na changamoto zinazozikabili sekta hizi. Uongozi wa Wizara umewaahidi wadau hao kushirikiana katika kuimarisha sekta hizi, kwani ni vyema kuzishirikisha sekta binafsi katika kufikia malengo ya nchi.

88. **Mheshimiwa Spika,** Idara imetayarisha na kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa mwaka 2019/2020 pamoja na Mpango Kazi wa mwaka 2020/2021 kwenye kikao maalumu cha Bango Kitita kilichofanyika Ikulu katika uongozi wa awamu ya saba. Pia, Idara imetayarisha na kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi aliyoyatoa wakati alipowaapisha Waheshimiwa Mawaziri na Makatibu Wakuu, vikao hivyo vimewashirikisha Watendaji Wakuu wa Wizara. Aidha, Idara imewasilisha ripoti ya Utekelezaji wa shughuli za kila siku pamoja na ripoti za Miradi ya Maendeleo Tume ya Mipango pamoja na kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa Ilani ya CCM katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

89. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021, programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 353,101,960/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2021 imefanikiwa kupata shilingi **123,231,062/=** sawa na **asilimia 34.90. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D).**

**Program Ndogo: Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

90. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba.

**91.** **Mheshimiwa Spika,** huduma ambazo zinatolewa ni uratibu wa Sera, Tafiti na Mipango Mikuu ya Ofisi Kuu Pemba, kuratibu Miradi ya Maendeleo na kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi.

**UTEKELEZAJI HALISI**

**92.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imeratibu shughuli za utafiti na kuendeleza kufanya vipindi vya Televisheni ya ZBC TV vinavyojulikana kama **Hazina iliyofichika,** Aidha, Ofisi Kuu imeratibu mikutano na wadau wa Utalii na Mambo ya Kale kwa lengo la kuhamasisha utalii wa ndani pamoja na kuyatunza na kuyalinda maeneo ya kihistoria na Mambo ya Kale yaliyopo Pemba. Pia, mikutano hiyo ilitoa fursa kwa wadau kusikilizwa changamoto zinazokabili sekta hizo pamoja na wao kuhimizwa kuwekeza katika sekta hizi kwani zinatoa fursa nyingi za ajira kwa vijana. Vile vile, Ofisi Kuu Pemba imefanya vikao vya kiutendaji sambamba na kufanya ziara katika maeneo ya kihistoria, vivutio vya kiutalii na miradi ya Maendeleo.

**93.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imegharamia mafunzo ya awali (Induction Course) kwa wafanyakazi sita wapya ambao hawakuwahi kupata mafunzo hayo. Mafunzo haya hutolewa na Chuo cha Utumishi wa Umma. Aidha, Wafanyakazi 19 wamelipwa stahiki zao za likizo na posho la muda wa ziada.

**94.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021, programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 844,832,640/=,** kwa ajili ya kazi za kawaida, hadi kufikia Machi 2021 imefanikiwa kupata **shilingi 532,310,682/=** sawa na **asilimia 63.01**. Programu hii imetakiwa kukusanya jumla ya **shilingi 40,197,000/=** hadi kufikia Machi 2021,

jumla ya **shilingi 371,500/=** zimekusanywa sawa na **asilimia 0.92**. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D na 1E).**

## J. MIRADI YA MAENDELEO ITAKAYOTEKELEZWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

95. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imepangiwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo ifuatayo: -

i. Mradi wa Kuyaimarisha maeneo ya Kihistoria.

Mradi huu utatekeleza shuguli zifuatazo: -

a. Kulifanyia matengenezo jengo la Mfalme wa Uingereza (British Residence) liliopo Chwaka Unguja
b. Kulifanyia matengenezo jengo la Afro Shirazi Part (ASP) liliopo kijangwani Unguja
c. Kuifanyia matengenezo nyumba ya kihitoria ya Wahindi iliyopo Fufuni Pemba
d. Kuufanyia matengenezo Msikiti wa kihistoria uliopo Kichokochwe Pemba
e. Kulifanyia matengenezo jengo la Ngome Kongwe liliopo Chake Chake Pemba

ii. Mradi wa Utalii kwa Wote.

Mradi huu utatekeleza shuguli zifuatazo: -

a. Kuendelea na shughuli za ujenzi katika kituo cha kivutio cha utalii kilichopo Bungi Unguja.

96. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na miradi ambayo Wizara imepanga kuitekeleza kwa mwaka wa fedha 2021/2022, pia, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyoanza utekelezaji wake mwaka wa fedha 2020/2021 ambayo mpaka sasa haijakamilika.

**97.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza sekta ya utalii Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imebuni miradi mikubwa ya uwekezaji na inaendelea kutafuta wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuanzisha na kuendeleza miradi hiyo. Miongoni mwa miradi hiyo ni ujenzi wa onesho la viumbe hai wa baharini (Oceanarium), ujenzi wa maegesho ya vyombo vya utalii wa baharini (marina), ujenzi wa bustani na utoaji wa huduma za kisasa zinazoendana na uhifadhi wa mazingira katika maeneo ya hifadhi (Waterfront and botanic garden) na ujenzi wa kituo cha kisasa cha utafiti wa kihistoria (Acheololigal Reseach center). Uwekezaji wa miradi hii kutasaidia juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu nane kwa kutoa ajira 300,000 ifikapo mwaka 2025.

**98.** **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha wazawa na wageni wote kuchangamkia fursa hii ya uwekezaji ili kuweza kujenga uchumi wa nchi yetu kwa pamoja.

## K. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**99.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022, Wizara ya Utalii, na Mambo ya Kale imepangiwa jumla ya **shilingi 12,882,900,000/=**. Kati ya fedha hizo **shilingi 7,382,900,000/=** kwa matumizi ya kawaida na **shilingi 5,500,000,000/=** kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, Wizara imepangiwa kukusanya mapato yanayokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali **shilingi 5,947,834,000/=. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1F, 1G, 1H, 1I).**

**100.** **Mheshimiwa Spika,** katika fedha za matumizi ya kawaida ambazo ni **shilingi 7,382,900,000/= shilingi 3,628,661,000/=** ni mishahara kwa taasisi za Wizara zisizo za ruzuku, **shilingi 2,917,739,000/=** kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa taasisi za Wizara zisizo za

ruzuku. Aidha, shilingi **492,300,000/=** kwa ajili ya mishahara kwa taasisi ya Wizara ya ruzuku na shilingi **344,200,000/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa taasisi za Wizara za ruzuku. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1F).**

101. **Mheshimiwa Spika,** katika fedha za miradi ya maendeleo s**hilingi 3,500,000,000/=** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria na **shilingi 2,000,000,000/=** kwa ajili ya Mradi wa Utalii kwa Wote. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1F).**

## L. KUWASILISHA BAJETI YA MFUMO WA PROGRAMU (PROGRAM BASED BUDGET - PBB) KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

102. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imepangiwa kutumia jumla ya **shilingi 12,882,900,000/=** kwa ajili ya kutekeleza programu kuu tano ambazo ni: -

i. Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii. **(Shilingi 277,784,000/=).**

ii. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale Nyaraka na Uhifadhi wa Mji Mkongwe. **(Shilingi 6,115,154,000/=).**

iii. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii. **(Shilingi 594,110,250/=).**

iv. Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii. **(Shilingi 3,448,789,750/=).**

v. Programu ya Utawala na Uendeshaji katika sekta ya Utalii na Mambo ya Kale. **(Shilingi 2,447,062,000/=). (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1H).**

## PROGRAMU YA KWANZA: (PJ0401) PROGRAMU YA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII.

103. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii inatekelezwa na Idara ya Utalii. Jukumu la msingi katika programu hii ni Kusimamia na Kuratibu shughuli za Utalii pamoja na Kuwahamasisha Wananchi juu ya dhana ya Utalii kwa Wote. Matokeo ya muda mrefu ni kuwa na Utalii wenye kuleta Manufaa kwa Wananchi. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni Uratibu na Uendelezaji wa shughuli za Utalii.

104. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022 programu hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kufanya utafiti wa kutambua uwezo wa kisiwa cha Zanzibar wa kuhimili idadi ya wageni wanaoingia nchini.
ii. Kutoa elimu kwa wananchi kupitia vyombo vya habari juu ya utekelezaji wa Sera ya Utalii.
iii. Kuendelea na Mpango wa usafi katika vivutio vya utalii.

105. **Mheshimiwa Spika,** ili programu hii iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 277,784,000/=** kwa kazi za kawaida.

## PROGRAMU YA PILI:(PJ0402) PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE.

**106.** **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa maeneo ya Kihistoria na Mambo ya Kale yanaendelezwa kwa kuhifadhiwa, kulindwa na kutangazwa. Aidha, kuwepo Usimamizi bora wa Kumbukumbu na Nyaraka kwa ajili ya matumizi ya Taifa pamoja na Kuuhifadhi na Kuuendeleza Mji Mkongwe ili uendelee kubaki kuwa urithi wa dunia kwa kutoa faida kwa kizazi cha sasa na baadae. Aidha, matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni Kuyaimarisha Maeneo ya Kihistoria, Kuwepo kwa Usimamizi Imara wa Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa pamoja na Kuuendeleza Mji Mkongwe. Programu hii imepangiwa jumla ya **shilingi 6,115,154,000/=** na itakuwa na programu ndogo mbili ambazo ni: -

i. Uendelezaji wa Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe **(Shilingi 5,453,872,000/=)**
ii. Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa **(Shilingi 661,282,000/=)**

### Programu Ndogo: (SJ040201) Uendelezaji wa Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe

**107.** **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Uendelezaji wa Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe inatekelezwa na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale pamoja na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe. Jukumu la msingi katika programu ndogo ni Kuimarisha, Kuendeleza na Kuyahifadhi Maeneo ya Kihistoria na Mambo ya Kale yaliyopo nchini pamoja na Mji Mkongwe. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni Kuendeleza Urithi wa Mambo ya Kale na Mji Mkongwe pamoja

na Uelimishaji na Ushirikishwaji wa Jamii katika Uhifadhi na Uendelezaji wa Maeneo ya Kihistoria

.

108. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kufanya Utafiti wa masimulizi (Oral History) pamoja na Utafiti wa Akiolojia.
ii. Kutoa Elimu kwa Jamii juu ya Umuhimu wa Kuyalinda na Kuyahifadhi Maeneo ya Kihistoria yaliyopo Nchini.
iii. Kutoa ushauri wa kitaalamu, kusimamia miradi ya Uhifadhi wa Majengo na maeneo ya wazi kwa mujibu wa Mpango Mkuu wa Uhifadhi (Conservation and Heritage Management Plan).
iv. Kushirikiana na Sekta binafsi katika uhifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe kwa kuufanya Mji huu kuwa kivutio zaidi cha utalii.

109. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 1,953,872,000/=** kwa kazi za kawaida na **shilingi 3,500,000,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria. Pia, programu hii imetakiwa kukusanya **shilingi 332,800,000/=**, zinazokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali.

**Program Ndogo: (SJ040202) Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa**

110. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa inatekelezwa na Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu ya Taifa Zanzibar. Jukumu la msingi katika programu ndogo hii ni Kuhifadhi na Kusimamia Nyaraka na Kumbukumbu

za Taifa. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni Kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa.

111. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuimarisha Uhifadhi na Utunzaji Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar.
ii. Kufanya Ukaguzi wa kumbukumbu na kutoa Elimu ya Utunzaji na Uhifadhi kumbukumbu kwa Taasisi za Umma na kuimarisha utoaji wa huduma kwa watafiti wa ndani na nje ya nchi.
iii. Kuhuisha Nyaraka kwa kuimarisha, kuhifadhi na kuendeleza Urithi wetu, Historia na Utamaduni kwa manufaa ya Taifa

112. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo iweze kufanya kazi zake katika mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 661,282,000/=** kwa kazi za kawaida na Makusanyo ya **shilingi 15,000,000/=,** zinazokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali.

**PROGRAMU YA TATU: (PJ0201) PROGRAMU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI UTALII.**

113. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuongeza uelewa kwa wakazi wa Tanzania na jamii ya kimataifa kuhusu bidhaa na huduma za utalii zilizopo Zanzibar. Programu inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi.

114. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022 programu hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo : -

i. Kuandaa na kushiriki maonesho, mikutano na makongamano ya utalii ya kitaifa na kimataifa ili kuvutia wageni kuvitembelea vivutio vya utalii vya Zanzibar.
ii. Kuwaalika waandishi wa habari za utalii wa kimataifa, wamiliki wa mitandao ya kijamii na watu mashuhuri ili Zanzibar imepata fursa ya kutangazwa kupitia watu hawa kwa gharama nafuu.
iii. Kuandaa na kutoa matangazo ya utalii katika majarida, televisheni za kitaifa na kimataifa na mabango ya kielektroniki, ili kuwavutia watalii wengi zaidi kutoka katika masoko ya asili na mapya.

**115. Mheshimiwa Spika,** ili programu hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 594,110,250/=** kwa kazi za kawaida.

## PROGRAMU YA NNE:(PJ0202) PROGRAMU YA KURATIBU NA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII.

**116. Mheshimiwa Spika,** programu hii ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii inatekelezwa na Idara ya Mipango na Sera kupitia Kamisheni ya Utalii, programu hii ina jukumu la Kuratibu, Kusimamia na Kuendeleza Utalii pamoja na Kuwajengea Uwezo Wafanyakazi na Kuweka Mazingira Mazuri ya Kazi.

**117. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kufanya ukaguzi wa miradi ya utalii na doria katika maeneo ya utalii.

ii. Kutoa mafunzo kwa watoa huduma za utalii ili kuboresha huduma wanazozitoa kwa wageni pamoja na mafunzo kwa masheha juu ya Sheria na kanuni za utalii.
iii. Kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu sekta ya utalii pamoja na fursa zinazopatikana kwa kutumia redio, televisheni na makongamano.

**118.** **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 1,448,789,750/=** kwa kazi za kawaida na **shilingi 2,000,000,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Utalii kwa Wote. Pia, programu hii imetakiwa kukusanya s**hilingi 5,575,000,000/=,** zinazokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali.

## PROGRAMU YA TANO: (PJ0403) UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YAUTALII NA MAMBO YA KALE

**119.** **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina jukumu la Kusimamia na Kuratibu Mipango Mikuu, Sera na Tafiti pamoja na Usimamizi na Uuendeshaji mzuri wa Rasilimali Watu katika Wizara. Matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa Usimamizi bora wa Mipango na Uendeshaji wa Rasilimali Watu katika Wizara. Programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 2,447,062,000/= na itasimamia programu ndogo tatu ambazo ni: -

i. Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale. **(Shilingi 1,601,118,000/=)**
ii. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara. **(Shilingi 260,431,000/=)**
iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba. **(Shilingi 585,513,000/=)**

**Program Ndogo: (SJ040301) Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.**

**120. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi, ambayo ina jukumu la Kusimamia shughuli zote za Utawala, Utumishi, Maendeleo, Wajibu na Maslahi ya Wafanyakazi wa Wizara.

**121. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo hii ni Usimamizi na Uendeshaji mzuri wa Rasilimali Watu wa Wizara. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni Kujenga uwezo na Mazingira Mazuri ya Kazi kwa Wafanyakazi na Usimamizi wa Mpango wa Manunuzi na Fedha.

**122. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuwajenga uwezo wafanyakazi pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kufanya kazi.
ii. Kupima utendaji kazi wa wafanyakazi wa Wizara kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wa Wizara;
iii. Usimamizi wa mpango wa manunuzi na utayarishaji wa ripoti za ukaguzi wa ndani.
iv. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA na Habari katika shughuli za Wizara.
v. Kuimarisha Mashirikiano baina ya Wadau, Wizara, Taasisi na Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa kwa ajili ya Maendeleo ya nchi.

**123.** **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 1,601,118,000/=** kwa kazi za kawaida.

**Programu Ndogo:(SJ040302) Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara.**

**124.** **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la Kupanga, Kutayarisha, Kuratibu, Kufuatilia na Kutathmini Mipango, Sera, Tafiti na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

**125.** **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo ni Kusimamia na Kuratibu Mipango Mikuu, Sera na Tafiti za Wizara. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni Uratibu wa Sera na Tafiti, Kuratibu, Kuandaa Bajeti pamoja na Kuratibu na Kusimamia Mipango na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

**126.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuandaa Mpango Mkakati wa Wizara (Strategic Plan)
ii. Kufanya mapitio ya Sera ya Urithi wa Mambo ya Kale, Sera ya Utunzaji wa Nyaraka na Sera ya Utalii.
iii. Kufuatilia na Kutathmini utekelezaji wa Malengo na Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara.
iv. Kuratibu Vikao vya Ushirikiano kwa sekta ya Utalii na Mambo ya Kale baina ya SMZ na SMT.

**127. Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2021/2021, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla **shilingi 260,431,000/=** kwa kazi za kawaida.

**Programu Ndogo: (SJ040303) Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba.**

**128. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba, ina jukumu la Kuhakikisha kuwa Majukumu, Malengo na shughuli zote za Wizara zilizopangwa zinatekelezwa kwa ufanisi kwa upande wa Pemba.

**129. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo ni Kusimamia na Kuratibu shughuli za Utawala, Uendeshaji na Mipango Mikuu ya Wizara katika Ofisi Kuu-Pemba. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni Uratibu wa Sera, Tafiti na Mipango Mikuu ya Ofisi Kuu-Pemba, Kuratibu Miradi ya Maendeleo na Kuwajengea Uwezo Wafanyakazi na Mazingira mazuri ya kazi.

**130. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuratibu shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba.
ii. Kupima utendaji kazi kwa Wafanyakazi wa Wizara Pemba kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kazi.
iii. Kufuatilia na Kutathmini utekelezaji wa Malengo na Miradi inayotekelezwa Pemba
iv. Kuwapatia Wafanyakazi vitendea kazi vya kutosha ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

**131.** **Mheshimiwa Spika,** ili programu hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 585,513,000/=** kwa kazi za kawaida na makusanyo ya **shilingi 25,034,000/=** zinazokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali.

## M. SHUKURANI

**132.** **Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba kutoa shukurani za kipekee kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa njia bora anazozitumia za kuiongoza vyema nchi yetu katika misingi ya Uwazi na Utawala Bora pamoja na kuhakikisha maendeleo ya nchi yanapatikana kwa maslahi mapana ya wananchi. Pia, ninaendelea kumshukuru kwa miongozo anayotupa katika kuhakikisha sekta ya Utalii na Mambo ya Kale inapiga hatua kubwa ya kimaendeleo, ninamuombea kwa Mwenyezi Mungu amzidishie ujasiri katika utendaji wake wa kazi.

**133.** **Mheshimiwa Spika,** shukurani maalumu ziwaendee waliochangia katika kutayarisha hotuba hii na wasaidizi wangu wa karibu katika Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Bi. Fatma Mabrouk Khamis, Afisa Mdhamini Pemba pamoja na Wakurugenzi na Wakuu wote wa Taasisi za Wizara kwa kufanya kazi kwa Juhudi, Maarifa, Uadilifu na Umakini Mkubwa. Kwa kweli wamekuwa wakinisaidia sana kutekeleza majukumu yangu. Pia, nawashukuru wafanyakazi wote wa Wizara Unguja na Pemba kwa kujituma zaidi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku na kuhakikisha wanakwenda sambamba na kasi ya utendaji ya Serikali ya awamu ya nane.

**134.** **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee naomba kuwashukuru wadau wote katika sekta ya Utalii na Mambo ya Kale wa Unguja

na Pemba kwa jinsi tunavyoshirikiana nao bega kwa bega katika kuhakikisha sekta hizi zinapata maendeleo makubwa kwa haraka.

135. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kuishukuru Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Tume ya Mipango kwa ushirikiano mkubwa waliotupa kwa mahitaji ya fedha na ushauri kwa kipindi chote tunapohitaji.

136. **Mheshimiwa Spika,** naomba uniruhusu nizishukuru nchi na mashirika ambayo yameshirikiana kwa karibu na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, katika kufanikisha kutekeleza Malengo na Majukumu ya Wizara kupitia sekta zake. Miongoni mwa nchi hizo ni pamoja na Oman, Saudia Arabia, India, Urusi. Pia, Shirika la UNDP, pamoja na Mabalozi wote wanaoiwakilisha Tanzania nje ya nchi.

137. **Mheshimiwa Spika,** mwisho naomba kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa Utulivu, Umakini na Usikivu wa hali ya juu.

## N. MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

138. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu lijadili kwa kina matumizi ya jumla ya Wizara ya **shilingi 12,882,900,000/=.** Kati ya hizo **shilingi 7,382,900,000/=** kwa kazi za kawaida na **shilingi 5,500,000,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Katika jumla kuu ya Wizara limo fungu la fedha la Kamisheni ya Utalii ambalo ni **shilingi 2,042,900,000/=** kwa kazi za kawaida na **shilingi 2,000,000,000/=** kwa ajili ya kutekeleza mradi wa Utalii

kwa Wote. Aidha, naliomba Baraza lako liidhinishe makusanyo ya mapato ya **shilingi 5,947,834,000/=** kwa fedha zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

## O. HITIMISHO

**139. Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima nawaomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu Waipokee, Waijadili, Watushauri, Watuelekeze na baadae Watupitishie bajeti hii ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.

**140. Mheshimiwa Spika,** Naomba Kutoa Hoja.



**Mheshimiwa; Lela Muhamed Mussa (MBM)**
**Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale.**

# VIAMBATISHO

**KIAMBATISHO 1A**

**MCHANGANUO KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

| TAASISI/IDARA | MAELEZO | BAJETI YA JULAI 2020 - 2021 | FEDHA ZILIZOPATIKA NA JULAI - MACHI 2020/2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| Ofisi kuu Pemba | Mishahara | 634,832,640.00 | 451,076,640.00 | 71.05 |
| | M/Mengineyo | 210,000,000.00 | 81,234,042.00 | 38.68 |
| JUMLA | | 844,832,640.00 | 532,310,682.00 | 63.01 |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | 103,101,960.00 | 78,315,215.00 | 75.96 |
| | M/Mengineyo | 250,000,000.00 | 44,915,847.00 | 17.97 |
| JUMLA | | 353,101,960.00 | 123,231,062.00 | 34.90 |
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | Mishahara | 1,074,717,420.00 | 704,406,100.00 | 65.54 |
| | M/Mengineyo | 873,016,550.00 | 270,761,235.00 | 31.01 |
| JUMLA | | 1,947,733,970.00 | 975,167,335.00 | 50 |
| Idara ya Utalii | Mishahara | 108,149,700.00 | 112,313,945.00 | 103.85 |
| | M/Mengineyo | 120,000,000.00 | 28,999,605.00 | 24.17 |
| JUMLA | | 228,149,700.00 | 141,313,550.00 | 61.94 |
| Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu | Mishahara | 418,202,460.00 | 350,556,795.00 | 83.82 |
| | M/Mengineyo | 250,000,000.00 | 54,621,957.00 | 21.85 |
| | | 668,202,460.00 | 405,178,752.00 | 60.64 |
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | Mishahara | 804,417,000.00 | 676,878,380.00 | 84.15 |
| | M/Mengineyo | 270,000,000.00 | 78,721,686.00 | 29.16 |
| JUMLA | | 1,074,417,000.00 | 755,600,066.00 | 70.33 |
| Kamisheni ya Utalii | Mishahara | 780,500,000.00 | 545,472,060.00 | 69.89 |
| | M/Mengineyo | 1,334,800,000.00 | 335,000,575.00 | 25.10 |
| JUMLA | | 2,115,300,000.00 | 880,472,635.00 | 41.62 |
| **JUMLA MISHAHARA** | | **3,923,921,180.00** | **2,919,019,135.00** | **74.39** |
| **JUMLA MATUMIZI MENGINEYO** | | **3,307,816,550.00** | **894,254,947.00** | **27.03** |
| **JUMLA KUU KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU** | | **7,231,737,730.00** | **3,813,274,082.00** | **52.73** |

**KIABATISHO 1B**

**MCHANGANUO WA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021 KWA TAASISI ZA RUZUKU**

| TAASISI/IDARA | MAELEZO | BAJETI YA JULAI 2020 - 2021 | FEDHA ZILIZOPATIKA NA JULAI - MACHI 2020/2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | Mishahara | 474,950,000.00 | 357,302,650.00 | 75.23 |
| | M/Mengineyo | 445,030,598.00 | 88,526,166.00 | 19.89 |
| | | 919,980,598.00 | 445,828,816.00 | 48.46 |
| **JUMLA YA MISHAHARA YA RUZUKU** | | **474,950,000.00** | **357,302,650.00** | **75.23** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO** | | **445,030,598.00** | **88,526,166.00** | **19.89** |
| **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **919,980,598.00** | **445,828,816.00** | **48.46** |
| | | | | |
| | | | | |
| **JUMLA YA MISHAHARA KWA WIZARA** | | **4,398,871,180.00** | **3,276,321,785.00** | **74.48** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO KWA WIZARA** | | **3,752,847,148.00** | **982,781,113.00** | **26.19** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA (MATUMIZI YA KAWAIDA)** | | **8,151,718,328.00** | **4,259,102,898.00** | **52.25** |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | | | | |
| Kuimarisha maeneo ya kihistoria | | **2,700,000,000.00** | **1,004,996,904.69** | **37.22** |
| Kuimarisha Utalii kwa wote | | **2,000,000,000.00** | **352,253,708.00** | **17.61** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA (MIRADI YA MAENDELEO)** | | **4,700,000,000.00** | **1,357,250,612.69** | **28.88** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA** | | **12,851,718,328.00** | **5,616,353,510.69** | **43.70** |

**KIAMBATISHO 1C**

**MAPATO YALIOKUSANYWA JULAI 2020 HADI MACHI 2021**

**MAPATO YANAYOINGIA HAZINA**

| TAASISI | BAJETI 2020/2021 | MAPATO YALIOKUSANYWA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale** | 245,031,000.00 | 62,519,474.00 | **25.51** |
| **Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu** | 7,094,000.00 | 116,150.00 | **1.64** |
| **Ofisi Kuu Pemba** | 40,197,000.00 | 371,500.00 | **0.92** |
| **Mamlaka ya Mji Mkongwe** | 30,000,000.00 | 43,500,000.00 | **145.00** |
| **JUMLA NDOGO** | **322,322,000.00** | **106,507,124.00** | **33.04** |
| **Kamisheni ya Utalii** | 5,492,029,000.00 | 3,226,297,078.00 | **58.75** |
| **JUMLA NDOGO** | **5,492,029,000.00** | **3,226,297,078.00** | **58.75** |
| **JUMLA** | 5,814,351,000.00 | 3,332,804,202.00 | **57.32** |

**KIAMBATISHO 1D**

**FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 KWA KILA PROGRAMU NDOGO**

**Programu ndogo ya Uendelezaji wa Urithi wa Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale** | 3,774,417,000.00 | 1,760,596,970.69 | **46.65** |
| **Mamlaka ya Mji Mkongwe** | 919,980,598.00 | 445,828,816.00 | **48.46** |
| **JUMLA** | **4,694,397,598.00** | **2,206,425,786.69** | **47.00** |

**Programu ndogo ya Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa**

| TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MARCH2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu** | 668,202,460.00 | 405,178,752.00 | **60.64** |
| **JUMLA** | **668,202,460.00** | **405,178,752.00** | **60.64** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kuendeleza Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MARCH2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Idara ya Utalii** | 228,149,700.00 | 141,313,550.00 | **61.94** |
| **JUMLA** | **228,149,700.00** | **141,313,550.00** | **61.94** |

**Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MARCH2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Kamisheni ya Utalii(Idara ya Masoko)** | 602,830,000.00 | 99,437,250.00 | **16.50** |
| **JUMLA** | 602,830,000.00 | 99,437,250.00 | **16.50** |

**Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MARCH2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Kamisheni ya Utalii(Idara ya Mipango)** | 3,512,470,000.00 | 1,133,289,093.00 | **32.26** |
| **JUMLA** | 3,512,470,000.00 | 1,133,289,093.00 | **32.26** |

**Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MARCH2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Idara ya Uendeshaji na Utumishi** | 1,947,733,970.00 | 975,167,335.00 | **50.07** |
| **JUMLA** | 1,947,733,970.00 | 975,167,335.00 | **50.07** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara**

| TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MARCH2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Idara ya Mipango Sera na Utafiti** | 353,101,960.00 | 123,231,062.00 | **34.90** |
| **JUMLA** | 353,101,960.00 | 123,231,062.00 | **34.90** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MARCH2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Ofisi Kuu Pemba** | 844,832,640.00 | 532,310,682.00 | **63.01** |
| **JUMLA** | 844,832,640.00 | 532,310,682.00 | **63.01** |

**KIAMBATISHO 1E**
**FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 KWA KILA PROGRAMU NDOGO**

**Programu ndogo ya Uendelezaji wa Urithi wa Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale** | 245,031,000.00 | 62,519,474.00 | **25.51** |
| **Mamlaka ya Mji Mkongwe** | 30,000,000.00 | 43,500,000.00 | **145.00** |
| **JUMLA** | **275,031,000.00** | **106,019,474.00** | **38.55** |

**Programu ndogo ya Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa**

| TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MARCH2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu** | 7,094,000.00 | 116,150.00 | **1.64** |
| **JUMLA** | **7,094,000.00** | **116,150.00** | **1.64** |

**Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MARCH2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Kamisheni ya Utalii(Idara ya Mipango)** | 5,492,029,000.00 | 3,226,297,078.00 | **58.75** |
| **JUMLA** | **5,492,029,000.00** | **3,226,297,078.00** | **58.75** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Ofisi Kuu Pemba** | 40,197,000.00 | 371,500.00 | **0.92** |
| **JUMLA** | **40,197,000.00** | **371,500.00** | **0.92** |

**KIAMBATISHO 1F**
**BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU**

| TAASISI/IDARA | MAELEZO | BAJETI YA JULAI-JUNI 2021-2022 |
|---|---|---|
| Ofisi kuu Pemba | Mishahara | 435,513,000.00 |
| | M/Mengineyo | 150,000,000.00 |
| JUMLA | | 585,513,000.00 |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | 110,431,000.00 |
| | M/Mengineyo | 150,000,000.00 |
| JUMLA | | 260,431,000.00 |
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | Mishahara | 711,079,000.00 |
| | M/Mengineyo | 890,039,000.00 |
| JUMLA | | 1,601,118,000.00 |
| Idara ya Utalii | Mishahara | 197,784,000.00 |
| | M/Mengineyo | 80,000,000.00 |
| JUMLA | | 277,784,000.00 |
| Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu | Mishahara | 504,721,000.00 |
| | M/Mengineyo | 156,561,000.00 |
| JUMLA | | 661,282,000.00 |
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | Mishahara | 948,772,000.00 |
| | M/Mengineyo | 168,600,000.00 |
| JUMLA | | 1,117,372,000.00 |
| Kamisheni ya Utalii | Mishahara | 718,800,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| | M/Mengineyo | 1,324,100,000.00 |
| JUMLA | | 2,042,900,000.00 |
| **JUMLA MISHAHARA** | | **3,627,100,000.00** |
| **JUMLA MATUMIZI MENGINEO** | | **2,919,300,000.00** |
| **JUMLA KUU KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU** | | **6,546,400,000.00** |

**KIAMBATISHO 1G**
**TAASISI ZA RUZUKU**

| TAASISI/IDARA | MAELEZO | BAJETI YA JULAI-JUNI 2021-2022 |
|---|---|---|
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | Mishahara | 492,300,000.00 |
| | M/Mengineyo | 344,200,000.00 |
| | | 836,500,000.00 |
| **JUMLA YA MISHAHARA YA RUZUKU** | | **492,300,000.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEO** | | **344,200,000.00** |
| **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **836,500,000.00** |
| | | |
| | | |
| **JUMLA YA MISHAHARA KWA WIZARA** | | **4,119,400,000.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO KWA WIZARA** | | **3,263,500,000.00** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA (MATUMIZI YA KAWAIDA)** | | **7,382,900,000.00** |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | | |
| Kuimarisha maeneo ya kihistoria | | **3,500,000,000.00** |
| Kuimarisha Utalii kwa wote | | **2,000,000,000.00** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA (MIRADI YA MAENDELEO)** | | **5,500,000,000.00** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA** | | **12,882,900,000.00** |

**KIAMBATISHO 1H**
**BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**Programu ndogo ya Uendelezaji wa Urithi wa Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2021/2022 MATUMIZI | BAJETI 2021/2022 MAPATO |
|---|---|---|
| **Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale** | 4,617,372,000.00 | 242,800,000.00 |
| **Mamlaka ya Mji Mkongwe** | 836,500,000.00 | 90,000,000.00 |
| **JUMLA** | **5,453,872,000.00** | **332,800,000.00** |

**Programu ndogo ya Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa**

| TAASISI | BAJETI 2021/2022 MATUMIZI | BAJETI 2021/2022 MAPATO |
|---|---|---|
| **Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu** | 661,282,000.00 | **15,000,000.00** |
| **JUMLA** | **661,282,000.00** | **15,000,000.00** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kuendeleza Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2021/2022 MATUMIZI | BAJETI 2021/2022 MAPATO |
|---|---|---|
| **Idara ya Utalii** | 277,784,000.00 | **-** |
| **JUMLA** | **277,784,000.00** | **-** |

## Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii

| TAASISI | BAJETI 2021/2022 MATUMIZI | BAJETI 2021/2022 MAPATO |
|---|---|---|
| **Kamisheni ya Utalii (Idara ya Masoko)** | 594,110,250.00 | - |
| **JUMLA** | **594,110,250.00** | **-** |

**Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2021/2022 MATUMIZI | BAJETI 2021/2022 MAPATO |
|---|---|---|
| **Kamisheni ya Utalii (Idara ya Mipango)** | 3,448,789,750.00 | 5,575,000,000.00 |
| **JUMLA** | **3,448,789,750.00** | **5,575,000,000.00** |

**Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2021/2022 MATUMIZI | BAJETI 2021/2022 MAPATO |
|---|---|---|
| **Idara ya Uendeshaji na Utumishi** | 1,601,118,000.00 | |
| **JUMLA** | **1,601,118,000.00** | **-** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara**

| TAASISI | BAJETI 2021/2022 MATUMIZI | BAJETI 2021/2022 MAPATO |
|---|---|---|
| **Idara ya Mipango Sera na Utafiti** | 260,431,000.00 | - |
| **JUMLA** | **260,431,000.00** | **-** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| TAASISI | BAJETI 2021/2022 MATUMIZI | BAJETI 2021/2022 MAPATO |
|---|---|---|
| **Ofisi Kuu Pemba** | 585,513,000.00 | 25,034,000.00 |
| **JUMLA** | **585,513,000.00** | **25,034,000.00** |

**KIAMBATISHO 1I**
**MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**MAPATO YANAYOINGIA HAZINA**

| **TAASISI** | **BAJETI 2021/2022** |
|---|---|
| **Mamlaka ya Mji Mkongwe** | 90,000,000.00 |
| **Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale** | 242,800,000.00 |
| **Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu** | 15,000,000.00 |
| **Ofisi Kuu Pemba** | 25,034,000.00 |
| **JUMLA NDOGO** | 372,834,000.00 |
| **Kamisheni ya Utalii** | 5,575,000,000.00 |
| **JUMLA NDOGO** | 5,575,000,000.00 |
| **JUMLA** | 5,947,834,000.00 |

**KIAMBATISHO NAMBA 2:**

**WAFANYAKAZI WA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE AMBAO WAMEKWENDA MASOMONI KWA MWAKA 2019/2020**

| S/N | Jina Kamili | Jinsi | Taasisi | Fani | Kiwango | Muda | Chuo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Nd. Zuwena Amour Sleiman | Mke | Uendeshaji na Utumishi | Uhusiano wa Kimataifa | Stashahada ya Uzamili | Mwaka 1 | CRF |
| 2. | Nd. Naomi Kurwa Shija | Mke | Uendeshaji na Utumishi | Utunzaji Kumbukumbu | VETA | Miaka 2 | ICPS |
| 3. | Nd. Zuhura Khamis Ambar | Mke | Uendeshaji na Utumishi | Utunzaji Kumbukumbu | Cheti | Mwaka 1 | ICPS |
| 4. | Nd. Ali Juma Ameir | Mme | Idara ya Makumbusho na Mambo ya | Art in Archaelogy | Shahada ya 2 | Miaka 2 | UDSM |
| 5. | Nd. Bakari Abdalla Sheha | Mme | Makumbusho na Mambo ya Kale | Lumber | Cheti | Mwaka 1 | ZAWA |
| 6. | Nd. Salma Suleiman Makenzi | Mke | Kamisheni ya/Utalii | Rasimali Watu | Shahada ya 1 | Miaka 3 | MNMA |
| 7. | Nd. Mauwa Juma Ali | Mke | Kamisheni ya/Utalii | Record And Archieve Management | Diploma | Miaka 2 | ICPS |
| 8. | Nd. Abdillah Faki Abassi | Mme | Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe | Uhandisi Umeme | Shahada ya 1 | Miaka 4 | KIST |
| 9. | Nd. Latifa Shaib Khamis | Mke | Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe | Uhandisi Ujenzi | Shahada ya 1 | Miaka 4 | Chuo cha Ardhi Dar-es--Salaam |
| 10 | Said Juma Haji | Mme | Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe | Uhandisi Ujenzi | Stashahada | Miaka 2 | KIST |
| 11 | Adam Ame Hamza | Mme | Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe | Sheria | Cheti | Mwaka 1 | ZLRS |
| 12 | Amina Mtumwa Ramadhan | Mke | Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe | Mawasiliano ya Habari | Stashahada | Miaka 2 | ICPS |
| 13 | Nd. Fatma Abass Khamis | Mke | Uendeshaji na Utumishi (Pemba) | Uchumi | Shahada 1 | Miaka 2 | ZU |

| S/N | **Jina Kamili** | **Jinsi** | **Taasisi** | **Fani** | **Kiwango** | **Muda** | **Chuo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 14. | Abdalla Salim Ali | Mme | Uendeshaji na Utumishi (Pemba) | Utawala wa Umma | Stashahada | Miaka 2 | IPA |
| 15. | Suleiman Seif Handhari | Mme | Uendeshaji na Utumishi (Pemba) | Government and Leadeship | Stashahada | Miaka 2 | OUT |

**KIAMBATISHO NAMBA 3:**

## ORODHA YA NYUMBA NA WAMILIKI ZILIZOPO MJI MKONGWE

| **Mmiliki** | **Idadi ya Nyumba zote** | **Idadi ya Nyumba zilizo katika hali mbaya** | **Nyumba ambazo ziko katika hali mbaya sana (hazikaliki)** |
|---|---|---|---|
| Shirika la nyumba | 365 | 37 | 15 |
| Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. | 405 | 22 | 6 |
| Watu binafsi | 1,673 | 59 | 14 |
| Taasisi za Serikali | 257 | 9 | 1 |
| **Jumla** | **2,700** | **127** | **36** |